# PBZ BANK

## BENKI YA WATU WA ZANZIBAR LTD (PBZ)

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MUDA MAALUM (BATCH II) ZA SALES OFFICER

**UTANGULIZI**

Benki ya Watu wa Zanzibar Limited (PBZ) ni benki ya kibiashara inayomilikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa asilimia 100%. Benki inaendelea kutoa huduma bora za kifedha kwa wateja wake Zanzibar na Tanzania Bara.

Katika jitihada zake za kuimarisha upanuzi wa huduma na kukuza mauzo ya bidhaa zake, PBZ inakaribisha maombi kutoka kwa vijana wenye ari, ubunifu na uwezo mzuri wa kushawishi wajiunge na Benki kwa nafasi ya **Mauzo (Sales)** katika idara ya Masoko kwa **mkataba wa muda maalum** kulingana na mahitaji ya Benki.

**NAFASI:** Afisa Mauzo (Sales Officer) - Nafasi 26

**MAENEO YA KAZI:**

Matawi na vituo mbalimbali vya PBZ - Zanzibar:

1. Forodhani Branch - 2
2. Malindi Branch - 2
3. Mlandege Branch - 2
4. IB Mpirani Branch - 2
5. Mwanakwerekwe Branch - 2
6. IB Amani Branch - 2
7. Chake Chake Branch - 2
8. IB Chake Branch - 2
9. Wete Branch - 2
10. Mkoani - 2
11. Paje - 1
12. Nungwi - 2
13. Kinyasini - 1
14. Konde - 1
15. Kiwengwa - 1

**MAJUKUMU YA KAZI:**

- Kutangaza na kuuza bidhaa na huduma za Benki kwa wateja wapya na waliopo.
- Kuwahamasisha wateja kufungua akaunti na kutumia bidhaa za Benki.
- Kutoa maelezo sahihi kwa wateja kuhusu huduma za PBZ na kuhakikisha wateja wanaridhika.
- Kuhusika na shughuli zote za mauzo na masoko.
- Kufikia malengo ya mauzo yaliyowekwa na kuwasilisha taarifa za utendaji kwa wakati.

**SIFA ZA MUOMBAJI:**

- Awe Mtanzania (wenye asili ya Zanzibar wanahimizwa zaidi kuomba).
- Mwenye umri usiozidi miaka 35
- Awe na Shahada katika fani za Masoko, Biashara, Uhasibu, Uchumi, Benki, Mahusiano ya Kimataifa au fani nyingine zinazohusiana.
- Awe na uwezo mzuri wa kuwasiliana na kushirikiana na watu.
- Awe na ari ya kazi, mshawishi, na mwenye lengo la kufikia matokeo.
- Awe tayari kufanya kazi kwa kujitegemea na katika mazingira yenye changamoto.

- Awe tayari kufanya kazi katika maeneo yoyote na muda wowote utakaohitajika.
- Awe si mwajiriwa wa Serikali kwa sasa.
- Awe tayari kufanya kazi kwa zamu au nje ya muda wa kawaida pale itakapohitajika.
- Awe na vyeti halisi vya kumalizia masomo, Cheti cha Kuzaliwa na CV.

**UWEZO NA SIFA BINAFSI (COMPETENCIES):**

- Ubunifu na uwezo wa kutatua changamoto kazini.
- Kujituma na kuwa na shauku ya kuuza na kuhudumia wateja.
- Nidhamu, uwajibikaji, na uaminifu kazini.

**JINSI YA KUOMBA:**

Maombi yote yawasilishwe kupitia barua pepe ifuatayo: **recruitment@pbzbank.co.tz** kuanzia tarehe **03 Septemba 2026** hadi tarehe **10 Septemba 2026.**
Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti ya PBZ ambayo ni **www.pbzbank.co.tz**

Waombaji wote wanatakiwa kuwasilisha:

- **Barua ya maombi ya kazi,**
- **Wasifu binafsi (CV),**
- **Nakala za vyeti vya taaluma, na**
- **Cheti cha kuzaliwa.**

Waombaji waliofanikiwa wanaweza kupangiwa kufanya kazi katika tawi au kituo chochote cha PBZ kulingana na mahitaji ya Benki.

Muombaji atakaewasilisha **"Progressive Report" au "Statement of Result"** maombi yake hayatozingatiwa.

Ahsante,

**IMETOLEWA:**
**MKURUGENZI MWENDESHAJI,**
**BENKI YA WATU WA ZANZIBAR,**
**S.L.P 1173,**
**ZANZIBAR.**